**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MASHUJAA SINZA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**Namba za Simu**
**Mkuu wa Shule: 0683 314093**
**Makamu Mkuu wa Shule: 0717 680568**
**Matron/Patron: 0621033246**
**Shule ya Sekondari: MASHUJAA SINZA**
**S.L.P: 90289,**
**DAR ES SALAAM**

**Tarehe: ……………**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**……………………………………………**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI <u>MASHUJAA SINZA</u> HALMASHAURI YA <u>MANISPAA YA UBUNGO</u> MKOA WA <u>DAR ES SALAAM</u> MWAKA <u>………………</u>**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka ……… na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya Sekondari **MASHUJAA SINZA** ipo umbali wa Kilometa **0.4** Mashariki mwa **Hospitali ya Sinza- Palestina** Kwa usafiri wa daladala, ukitokea kituo cha mabasi (daladala) cha **Makumbusho** au **Mwenge**, panda mabasi yanayoenda **gerezani/posta/mnazi mmoja,** kupitia barabara ya **Shekilango,** Nauli ni Shilingi **500** shuka kituo kinachoitwa **Palestina.**

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ……….. hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **……………..** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **………………..**

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni **Sketi mbili(2) za Dark blue** kwa Wasichana na **Suruali mbili (2) za Dark Blue** kwa Wavulana.

MSHONO:

Mshono wa suruali iwe na marinda mawili na mkunjo chini) isiwe ya kubana kwa chini.(UPANA inch 17)

Mshono wa sketi uwe wa V RINDA kwa mbele yenye urefu mpaka kwenye kisigino.

ii. Mashati **mawili (2) meupe ya mikono mifupi**

iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni **nyeupe** ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama

iv. Sare ya Michezo ni **Track Suti Moja(1) ya Dark Blue** Kwa wasichana na wavulana

v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

vi. Soksi ndefu jozi mbili **nyeupe** kwa wasichana na **nyeusi** kwa wavulana.

vii. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;

viii. Sweta moja ya Dark Blue kwa wasichana na wavulana.

ix. Tai ndefu mbili za dark blue kwa wavulana (sawa na rangi ya suruali) na SKAFU mbili za dark blue kwa wasichana (sawa na rangi ya sketi

x. Tisheti (T-shirt) ya Shule ya **Kijivu** aina ya **Form Six** itakayovaliwa siku ya Jumatano na Ijumaa.

**Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i) Madaftari counter book 4 quire 4.

ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatishwa*);

iv. Scientific Calculator; kwa Tahasusi yenye **Jiografia**

v. Kwanja 1 na Fagio 1 la Nje kwa Tahasusi ya HGL
Jembe 1 na Fagio 1 la Nje kwa Tahasusi ya HKL
Reki 1 na Fagio 1 la Ndani kwa Tahasusi ya HGK
Kwanja 1 na Fagio 1 la Nje kwa Tahasusi ya HKLi

### 2.2 Michango mbalimbali

a) **Shule za Kutwa**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 45,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| | **Jumla** | **50,000/=** |

Fedha zote zilipwe kwenye account namba:.**20510056073 NMB (JINA: MASHUJAA SEC**)

- Hakikisha unaandika jina kamili la E D mwanafunzi atakayelipiwa michango hiyo kwenye BPS ya benki.

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo shuleni.
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa ` kutunza simu ya mwanafunzi;**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka au kunyoa nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wasichana wanaruhusiwa kusuka nywele 5 – 7 za mnyoosho. Wavulana wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara au bangi;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
xix. Kucheza kamali

## 4. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv. Picha mbili(2) za wazazi au walezi wa mwanafunzi wanaoweza kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ……………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule: JOYCE A. KIVELEGE**

**Sahihi na Mhuri wa Mkuu wa Shule**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MASHUJAA SINZ
S. L. P 9028,
DAR ES SALAAM

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule : 0683 314093**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0717 680568**
- **Mwandamizi Taaluma : 0621033246**

**KIAMBATANISHO "A"**

**FOMU RASMI YA KUANDIKISHWA**

**A. SEHEMU HII IJAZWE NA MWANAFUNZI**

1. Jina kamili…………………………………………………………………………..
2. Uraia……………………………………………………………………………
3. Dini…………………………tarehe ya kuzaliwa………………………………
4. Mahali ulipozaliwa……………………….……………………………………
5. Yatima/sioyatima/mzazi mmoja (kata isiyohusika)…………………………
6. Shule uliyosoma kabla ya kujiunga na shule hii (jaza jedwali)

| SHULE ALIKOSOMA | MWAKA WA KUMALIZA |
|---|---|
| | |

Saini ya mwanafunzi ………………………Tarehe…………………………..

**B. SEHEMU HII IJAZWE NA MZAZI/MLEZI:**

1. Jina kamili la mzazi/mlezi…………………………………………………
2. Uraia……………………………………………………………………
3. Anuani kamili ……………..Mkoa……………………………Wilaya …………………………………………………………………………
4. Mtaa……………………………………………………………………….
5. Kata…………………………………………………………………………
6. Namba ya simu (ya haraka)…………………………………………...

**Kazi ya mzazi/mlezi**

1. Jina la mwajiri na idara…………………………………………………
2. Uraia……………………………………………………………………
3. Anuani……………………………………………………………………
4. Kazi ya Mzazi/Mlezi………………………………………………………..

Saini yaMzazi/Mlezi:……………………………Tarehe………………………………

**KIAMBATANISHO "B"**

**AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi………………………………………………………………………………………

1. Nimeyasoma na kuyaelewa maelezo yote na nimekubali kujiunga na shule ya sekondari MASHUJAA SINZA kuanzia ……………………………………
2. Naahidi kwamba:
   (a) Nitazingatia sheria zote na kutimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa.
   (b) Sitoshiriki katika vitendo vya hujuma wala vitendo ambavyo vitakuwa kinyume na taratibu za serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
   (c) Nitatunza mali ya umma ambayo ni pamoja na majengo, samani, vitabu na vifaa vya maabara.
   (d) Nipo tayari kuchukuliwa hatua yoyote stahiki endapo nitakiuka maelezo yaliyotolewa kwenye fomuhii.

**Saini ya mwanafunzi**…………………………**Tarehe**………………………………..

**AHADI YA MZAZI/MLEZI**

Mzazi/mlezi wa …………………………………………………..kidato cha V/VI

Naahidi kwamba:

(a) Nitashirikiana kikamilifu na uongozi wa shule na walimu wote kwa ujumla kumuelimisha na kumlea mtoto wangu. Hii pamoja na nikuhakikisha kuwa anazitii sheria zote za shule na kuyazingatia mambo yote muhimu yaliyotajwa.

(b) Nitafanya kila niwezalo kumwezesha mwanangu kufika shuleni kilasiku saa 12:30 asubuhi.

(c) Ninaruhusu mwanangu achukuliwe hatua yoyote stahiki atapovunja mojawapo ya sheria au kanuni zilizoorodheshwa .

**Saini ya Mzazi/Mlezi**……………………………. **Tarehe**…………………………

**UBUNGO MUNICIPAL COUCIL**
**SECONDARY EDUCATION DEPARTMENT**

**STUDENT'S MEDICAL EXAMINATION FORM**

**TO: THE MEDICAL OFFICER**

**HOSPITAL**:……………………………………………………………………………………
Student's Name……………………………………………Age…………… Sex…
Please examine the above named as to his/her fitness for appointment/re-engagement as a student at MASHUJAA SINZA SECONDARY SCHOOL

**MEDICAL CERTIFICATION**

(To be completed by a Medical Officer)

**(A)PHYSICAL EXAMINATION**

- Height…………………………………..
- Weight……………………………………
- Eye sight………………………………..
  Hearing…………………………………..…

**(B) PAST HISTORY**

- Heart diseases…………………………………………………………
- Drug allergy……………………………………………………………
- Diabetes………………………………………………………………
- Asthma…………………………………………………………………
- Pneumonia……………………………………………………………

**(C) LABORATORY TEST**

- Stool
- Urine
- Widal test
- VRDL
- Blood:
  B/S
  Hb
- Tuberculosis
- HIV

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit for appointment/re-engagement are as above.
Name of Authorized doctor…………………………………………………………..
Signature……………………Designation……………………………………………
Date…………………………Stamp…………………………………………….

## OORODHA YA VITABU KIDATO CHA TANO NA SITA.

A. HISTORY

1. TIE (2016) History for Secondary Schools: Form Five - Tanzania Institute of Education.
2. TIE (2016) History for Secondary Schools Form Six, Dar es Salaam: Tanzania Institute of Education
3. Tumaini, S.C.K (2010) Contemporary Historical Events: Advanced Level History one, Dar es Salaam: Shiibitali& Sons publishers
4. Yassin S. (..) Essentials in Advanced Levels History Paper 2, Dar es Salaam B. ENGLISH

B. LANGUAGE

1. Asheli, N. (2014) Advanced Level English: A Practical Approach,3rd Ed., Dar es Salaam: Good Books Publishers
2. John, J. (2012) Advanced English Language: Form 5 & 6, Dar es Salaam: Oxford University Press.
3. TIE (2016) English Language for Secondary Schools: Literature and Stylistics Form Five and Six, Dar es Salaam: Tanzania institute of Education

**POETRY**

a) Selected Poems. - Tanzania Institute of Education
b) The wonderful Surgeon and Other Poems. – Charles Mloka – Mkuki na Nyota Publishers Ltd.

**NOVELS AND SHORT STORIES (walau vitabu viwili)**

a) The Beautyful Ones Are Not Yet Born - AyiKweiArmah
b) A Man of the People - Chinua Achebe
c) Divine Providence - Severin N. Ndunguru
d) His Excellence Head of State - Danny Safo
e) Encounters from Africa – Macmillan Education Limited

PLAYS

a) Betrayal in the City - Francis Imbunga
b) I Will Marry When I Want – Ngugiwa Thiong’o and Ngugiwa Mirii
c) Lwanda Magere – Okoiti Omtatah
d) An Enemy of the People - Henrik Ibsen
e) Black Mamba - John Ruganda

C. GEOGRAPHY

1. Geography for Secondary Schools: Form Five. - Tanzania Institute of Education (2016)
2. Practical Geography: Map-reading, Photograph, Research and Surveying. – Zisti Kamili
3. Elementary Physical Geography: Advanced Level and Colleges. – Ahmed Lubwama
4. A Comprehensive Approach to Physical Geography – D.T. Msabila

## D. KISWAHILI

(i) KISWAHILI 1

1. Nadharia ya lugha ya Kiswahili1: Kidato cha Tano na Sita – Nyambari Nyangwine na Masebo (2010)
2. Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA): Sekondari naVyuo – Kihore, Y.M. na Masamba, D.P.B: TUKI (2003)
3. Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la pili: English – Swahili Dictionary – TUKI (ii) FASIHI
4. Nadharia ya FasihiKidato cha Tano na Sita – Masebo – Oxford university Press
5. Tahakiki Vitabu Teule Vya FasihiKidato cha 5 na 6 – Nyambari Nyangwinena Masebo
6. Nadharia ya lugha ya Kiswahili kidato cha tano na sita – Taasisi ya Elimu Tanzania

### TAMTHILIA

1. Kivuli Kinaish – Said Ahmed Mohamed – Oxford University Press
2. Kwenye Ukingowa Thimu – Ibrahim Hussein – Oxford University Press
3. Nguzo Mama – Penina Muhando (1982)
4. Morani –Emanuel Mbogo (1993)

### RIWAYA

1. Vutani Kuvute, 4th ed. – Mbunda Msokile (2009)
2. Kufikirika, 4th ed. – Shaban Robert – Mkukina Nyota
3. Mfadhili – Hussein Tuwa (2007) – Macmillan Aidan
4. Usiku Utakapokwisha, 2nd ed. – Mbunda Msokile (2007) – Macmillan Aidan

### USHAIRI

1. Kimbunga: Toleo la Tatu (3rd ed.) – Haji Gora Haji (1995) – TUKI
2. ChunguTamu – Theobald Mvungi
3. Mapenzi Bora – Shaban Robert – MkukinaNyota publishers
4. Fungate ya Uhuru – Mohamed S. Khatibu – Macmillan Aidan

## E. GENERAL STIUDIES

1. Nyangwine, C.M, Bukagile G.R &Maluka S.O (2010) Contemporary Approach for Advanced Level: General Studies Notes form 5 & 6. 2.
2. Bigirwamungu, J. & Deogratius S.M (2012) Understanding Advanced Level General Studies: Advanced Level Secondary Schools,
3. Mbalase Richard